MUUNDO WA KIRAI KITENZI KATIKA LAHAJA YA KITUMBATU

MWAJUMA NYANGE HAJI

TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (KISWAHILI) YACHUO KUKUU HURIA CHA TANZANIA

2018

UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapo chini anathibitisha kwamba, ameisoma tasnifu hii iitwayo: ***"Muundo Wa Kirai Kitenzi Katika Lahaja Ya Kitumbatu"*** na kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Digrii ya Uzamili katika Kiswahili (Isimu) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

……..

Dr. Hana Simpasa

(Msimamizi)

……..

Tarehe

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama kazi nzima au sehemu ya Tasnifu hii, isipokuwa /shughuli halali, kwa ajili ya utafiti, kujisomea, au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TAMKO

Mimi, **Mwajuma Nyange Haji,** nathibitisha kwamba tasinifu hii ni kazi yangu binafsi na halisi na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa, katika Chuo Kikuu kingine kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili au Shahada nyengine yoyote.

……

Saini

…….

Tarehe

TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabaruku kwa mume wangu mpenzi Bw Sheha Mjaja Juma na watoto wangu Maryam, Aisha, Zaynab na Khadija kwa mapenzi yao makubwa na ustahamilivu wa hali ya juu kwangu wakati wote wa kufanya utafiti huu.

SHUKRANI

Utafiti huu umefanyika kwa kuwashirikisha watu mbalimbali wa nje na ndani ya Tumbatu, hivyo wote wale ambao walifanikisha kukamilika kwa utafiti huo wanapewa shukurani za dhati kabisa. Napenda kutoa shukurani zangu kwa wakaazi wa Kisiwa cha Tumbatu hasa wale ambao walihusika kutoa taarifa za utafiti huu. Aidha, napenda pia kutoa shukurani maalum na za kipekee kwa msimamizi wangu Dkt Hanna Simpassa kwa muongozo na ushauri ambao alionipa wakati wote wa kufanya utafiti huu. Hakika muongozo na ushauri wake ndio ulifanikisha kukamilika kwa utafiti huu.

Shukurani nyengine naomba kuzitoa kwa walimu wangu wote wa Chuo Kikuu Huria ambao walifanikisha vizuri masomo yangu pamoja na wanafunzi wenzangu kwa mashirikiano yote waliyonipa tokea kunza kwa masomo hadi kumaliza. Nawashukuru kwa dhati kabisa Bibi Kijakazi Omar wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) na Bwana Mussa Khamis wa Skuli ya Sekondari ya Kiembesamaki kwa mashirikiano yote waliyonipa wakati wote nilipokuwa nikiwafuata.

Napenda pia kutoa shukurani kwa wafanyakazi wa Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA) kwa mashirikiano yote waliyonipa wakati nilipokwenda kwenye Baraza hilo. Kwa namna ya kipekee, naomba kutoa shukurani zangu za dhati kwa mume wangu mpendwa Nd. Sheha Mjaja Juma pamoja na watoto wangu wote (Maryam, Aisha, Zainab na Khadija) kwa ustahamilivu na upendo wao walionipa wakati wote wa masomo na wakati wa kufanya utafiti huu.

Kwa kuwa sio rahisi kuwataja wahusika wote ambao kwa njia moja ama nyengine waliweza kutoa ushirikiano wao uliosaidia kufanikisha utafiti huu, itoshe wote kwa pamoja wapokee shukurani zangu na Ahsanteni nyote.

IKISIRI

Utafiti huu unahusiana na muundo wa kirai kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu ambao umefanyika katika kisiwa cha Tumbatu ambapo ndio eneo halisi la wazungumzaji wa lahaja hiyo. Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza muundo wa virai vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu. Malengo mahususi ya utafiti huu ni kuchunguza ni vipashio gani vinavyoandamana na kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu, kuchunguza ni vipashio gani vinavyoandamana na kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu na kuchunguza ni kwa vipi virai vitenzi vya Kitumbatu vinaunda sentensi za Kitumbatu pamoja na kubainisha uelekezi unavyojitokeza katika vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu. Utafiti huu umehusisha watafitiwa wanawake na wanaume ambao ni watu wazima wenye umri wa miaka 70 na kuendelea, kati yao 13 ni wanawake na 12 ni wanaume ambao ni wakaazi wa Jongowe na Kichangani. Data za utafiti huu zilipatikana kutokana na hojaji zilizotayarishwa ambazo zilikuwa na maswali tafauti yaliyokuwa yanahusiana na virai vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu ambapo watafitiwa walitakiwa kujibu maswali yote ili data sahihi ziweze kupatikana. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa muundowa kirai kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu unavipashio vinavyoandamana navyo, vipashio hivyo ni kama vile nomino, kitenzi kisaidizi, kijalizi tegemezi na sentensi, kihusishi na kielezi. Utafiti huu umependekeza kuwa ufanyike utafiti mwengine unaohusu sarufiya lahaja ya Kitumbatu kwa kuchunguza vipengele mbali mbali vya kiisimu. Aidha utafiti umependekeza kuwa ufanyike utafiti ambao utaangalia tafauti ya matumizi ya lahaja ya Kitumbatu kati ya wanaume na wanawake.

YALIYOMO

UTHIBITISHO ..... **ii**

HAKIMILIKI ..... **iii**

TAMKO ..... **iv**

TABARUKU ..... **v**

SHUKRANI ..... **vi**

IKISIRI ..... **viii**

KIAMBATANISHO ..... **xii**

ORODHA YA VIFUPISHO ..... **xiii**

SURA YA KWANZA **1**

UTANGULIZI **1**

1.1 Usuli wa Mada 1

1.2 Tatizo la Utafiti 3

1.3 Malengo ya Utafiti 3

1.3.1 Lengo Kuu 3

1.3.2 Malengo Mahsusi 4

1.4 Maswali ya Utafiti 4

1.5 Umuhimu wa Utafiti 4

1.6 Mipaka/Mawanda ya Utafiti 5

1.7 Hitimisho 5

SURA YA PILI **6**

MAPITIO YA TAFITI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA **6**

2.1 Utangulizi 6

2.2 Mapitio na Machapisho 6

2.3 Tafiti zinazohusu Kitumbatu 6

2.2.2 Machapisho Katika Kiswahili Sanifu.....11

2.4 Kiunzi cha Nadharia.....13

2.3 Hitimisho 16

SURA YA TATU 17

MBINU ZA UTAFITI 17

3.1 Utangulizi 17

3.2 Eneo la Utafiti.....17

3.3 Sampuli ya Utafiti 18

3.4 Uteuzi wa Sampuli 18

3.5 Mbinu za Utafiti.....20

3.6 Faida na Hasara za Mbinu ya Hojaji ama Dodoso.....21

3.6.1 Faida Faida kubwa za Mbinu Hii ya Hojaji ama Dodoso ni Pamoja na: 21

3.7 Uchanganuzi wa Data.....22

3.8 Hitimisho 22

SURA YA NNE.....23

UWASLISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA.....23

4.1 Utangulizi 23

4.2 Matokeo ya Utafiti 23

4.2.1 Muundo na Vipashio wa Kirai Kitenzi cha Lahaja ya Kitumbatu.....23

4.2.2 Vipashio Vinavyoandama na Kirai Kitenzi cha Lahaja ya Kitumbatu 35

4.2.3 Sentensi za Lahaja ya Kitumbatu na Muundo Wake 36

4.2.3.1 Sentensi Sahili.....36

4.2.3.2 Sentensi Ambatano katika Kitumbatu.....38

4.2.3.3 Sentensi Changamani katika Lahaja ya Kitumbatu 39

4.2.4 Sentensi Changamani zenye Urejeshi 39

4.2.6 Sentensi Changamani Masharti.....40

4.2.7 Vitenzi Elekezi katika lahaja ya Kitumbatu 40

4.3 Hitimisho 44

SURA YA TANO.....45

MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, HITIMISHO LA JUMLA NA MAPENDEKEZO 45

5.1 Utangulizi 45

5.2 Muhtasari wa Utafiti.....45

5.3 Mapendekezo ya Utafiti 46

5.4 Hitimisho 46

MAREJELEO.....47

KIAMBATISHO.....49

KIAMBATANISHO

Kiambatisho I: Hojaji za Muundo wa Virai Vitenzi katika Lahaja ya Kitumbatu.....49

OORODHA YA VIFUPISHO

E	Kielezi
H	Kihusishi
KE	Kirai kielezi
KH	Kirai kihusishi
Kj	Kijalizo
KN	Kirai nomino
KT	Kirai kitenzi
N	Nomino
S	Sentensi
T	Kitenzi
Ts	Kitenzi Kisaidizi

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Tumbatu ni moja ya visiwa vichache vinavyokaliwa na watu ndani ya Kisiwa cha Zanzibar. Kisiwa hiki kipo Kaskazini mwa Unguja kilomita (48) kutoka Mjini Unguja na kilomita (3) kutoka Mkokotoni, kina urefu wa kilomita (15.5) na upana wa kilomita (2.5). Kisiwa cha Tumbatu kimegawika katika sehemu mbili ambazo ni Jongowe na Kichangani. Jongowe ipo upande wa kusini na Kichangani ipo upande wa Kaskazini mwa Kisiwa hicho. Kisiwa hiki kina historia kubwa kwa kuwa wenyeji wa Kisiwa hiki ambao wanaitwa Watumbatu wanajinasibisha na asili ya Zanzibar.

Kisiwa cha Tumbatu kipo katika Wilaya ya Kaskazini 'A' Unguja, Mkoa wa Kaskazini Unguja. Kisiwa hiki hivi sasa kimepewa hadhi ya kuwa Wilaya Ndogo inayojuilikana kwa jina la Wilaya ndogo ya Tumbatu. Wazungumzaji wakubwa wa lahaja ya Kitumbatu ni Watumbatu wenyewe wa visiwani ambapo asilimia kubwa ya msamiati, sauti, na matamshi hunasibishwa na wakaazi wa huko. Watumiaji wa lahaja ya Kitumbatu walioko nje ya Kisiwa hutumia sehemu ndogo ya msamiati huo, sauti na kiimbo chao hutafautiana kutoka sehemu moja na nyingine.

Lahaja ya Kitumbatu ni mojawapo ya lahaja ya Kiswahili inayozungumzwa katika eneo lote la Kisiwa cha Tumbatu na maeneo ya Kaskazini ya Kisiwa cha Unguja kama vile Nungwi, Potoa, Mkwajuni, Matemwe, Chaani, Mkokotoni, Mto wa Pwani, Pale na Donge. Hii ni lahaja ya Kiswahili ambayo haijafanyiwa utafiti wa kutosha, kazi chache zilizowahi kushughulikia lahaja hii ni kama vile utafiti uliofanywa na

Miraji na wenzake (2015) ambao uliangalia kupungua kwa matumizi ya lahaja ya Kitumbatu, nyingine ni utafiti uliofanywa na Makame (2012) ambao ulishughulikia muundo wa virai nomino katika lahaja ya Kitumbatu. Aidha kuna baadhi ya kamusi ambazo ni za lahaja ya Kitumbatu ambazo hutoa maana za maneno ya lahaja hii Hata hivyo.baadhi ya kazi hizo zimeshughulikia Kitumbatu kama ni sehemu ya kundi la lahaja kadhaa na si yenyewe peke yake.

Katika sintaksia kuna aina nyingi za maneno ikiwemo kategoria ya vitenzi ambayo ndiyo inayounda sentensi katika lugha mbali mbali ziliopo. Vitenzi ni aina ya maneno ambayo yana dhima kubwa. Habwe na Karanja(2004) wakimnukuu Mbaabu (1985) wanasema kuwa anavieleza Vitenzi kama ni maneno yoyote yanayoonyesha mambo yanayofanywa na watu wanyama , au vitu katika wakati fulani Pia hueleza hali fulani za watu ,vitu na matukio.

Pia Mgulu (1999) anaeleza kuwa vitenzi ni maneno pekee ambayo ni lazima yawepo katika sentensi ndipo sentensi iweze kuwa sentensi.PiaVitenzi vinaweza kukaa peke yake kama sentensi bila ya kusaidiwa na maneno mengine. Kwa mfano: Anaimba, alicheka, atasomesha, anakula n.k.

Aidha, katika lugha kuna vipashio ambavyo miongoni mwake kipo kijuilikanacho kama kirai. Kirai kimefafanuliwa kuwa ni neno au kifungu cha maneno ambacho hutoa taarifa fulani (Matinde 2012). Kwa kawaida kirai huwa hakina muundo wa kiima na kiarifu, kirai huweza kuundwa na neno pekee au neno linaloambatana na maneno mengine. Kwa kuwa katika mfumo wa lugha huwa kuna aina mbalimbali za maneno basi huwa pia kuna aina mbalimbali za virai kama vile virai nomino,

vivumishi, vitenzi, vielezi, virai vihusishi na kadhalika. Utafiti huu umechunguuza na kuchanganua muundo wa virai vitenzi katika lahaja ya Kiswahili ya Kitumbatu.

1.2 Tatizo la Utafiti

Wasomi wengi wamefanya utafiti wao kuhusu lahaja ya Kiswahili ya Kitumbatu kwa kuangalia vipengele mbalimbali vya kiisimu. Miongoni mwa wasomi hao ni . Kipacha (2003) ambaye amefanya utafiti unaohusiana na sifa bainifu za kifonolojia na ameeleza kuwa fonimu za Kitumbatu hazitafautiani na zile za Kiunguja. Miraji na wenzake (2012) waliangalia kuhusu kupungua kwa matumizi ya lahaja ya Kitumbatu.Vilevile Maganga (1990) alifanya utafiti juu ya mofofonolojia za lahaja ya Kiswahili akilinganisha maumbo hayo katika lahaja ya Kitumbatu. Pia Makame (2012) alifanya utafiti ulioangalia muundo wa virai nomino katika lahaja ya Kitumbatu.

Ingawa wasomi wengi wamejaribu kufanya tafiti zao katika lahaja ya Kitumbatu kwa kuangalia vipengele tafauti lakini kipengele cha virai tenzi vya lahaja ya Kitumbatu havijafanyiwa utafiti na msomi yoyote, kwa hiyo utafiti huu umeshughulikia kipengele hiki cha muundo wa virai tenzi katika lahaja ya Kitumbatu kwa undani zaidi.

1.3 Malengo ya Utafiti

1.3.1 LengoKuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguuza muundo wa kirai kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu.

1.3.2 Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi katika utafiti huu ni haya yafuatayo:

(i) Kuchunguza miundo na vipashio vinavyoandamana na kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu.

(ii) Kuchunguza miundo ya sentensi za lahaja ya Kitumbatu.

(iii) Kubainisha uelekezi unavyojitokeza katika vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu.

1.4 Maswali ya Utafiti

Masuala ya utafiti huu yaliyotumika ni:

(i) Kirai kitenzi cha Kitumbatu kina muundo gani na vipashio gani vinaandamana nacho?

(ii) Sentensi za lahaja ya Kitumbatu zina muundo gani?

(iii) Uelekezi katika vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu unajitokezaje?

1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu umesaidia kubainisha na kueleza muundo wa kipengele hiki cha kisarufi katika lahaja ya Kiswahili ya Kitumbatu kwa lengo la kuhamasisha na kuchochea tafiti nyingine katika uwanja wa vipengele mbalimbali vya kiisimu vya lahaja ya Kiswahili. Aidha, utafiti huu unatarajiwa kuwa na faida kubwa kwa kujaza pengo ambalo lipo kwa upande wa lahaja ya Kiswahili ya Kitumbatu la kutochunguzwa kwa kina vipengele vya kiisimu kuliko lahaja nyingine zilizopo upwa wa Afrika Mashariki. Utafiti huu vilevile utasaidia kuongeza wigo wa kuzielewa na kuzichambua ipasavyo lahaja nyingine za Kiswahili katika vipengele vyake ambavyo bado wasomi wanaendelea kuvichunguza.

Mwisho utafiti huu utasaidia kurekebisha baadhi ya kasoro zilizojitokeza katika baadhi ya tafiti zilizopita ambazo nyingi miongoni mwake hazikuwa za kina.

1.6 Mipaka/Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu umeshughulikia muundo wa kirai kitenzi katika lahaja ya Kiswahili ya Kitumbatu ambayo huzungumzwa katika eneo la Tumbatu. Aidha, utafiti huu umejikita kuchunguza vipashio vinavyoandamana na kitenzi ambavyo huwa vina muundo wake mahsusi. Kwa mfano sentensi zilizooneshwa ni kwa vipi kirai kitenzi kinaweza kuandamana na sentensi mbalimbali na umechunguza pia vipashio vya muundo wa kirai kitenzi pamoja na vibainishi vya muundo huo katika lahaja ya Kitumbatu.

1.7 Hitimisho

Kwa ujumla sura hii imejadili vipengele sita, ambavyo ni usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, umuhimu wa utafiti, maswali ya utafiti na mipaka ya utafiti ambapo vipengele hivi ndivyo vinavyoijenga sura ya kwanza katika kufanya utafiti.Sura ya pili inahusu mapitio ya tafiti tangulizi na kiunzi cha nadharia iliyotumika katika utafiti huu.

SURA YA PILI

MAPITIO YA TAFITI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii imegawanyika katika sehemu mbili : Sehemu ya kwanza inahusu mapitio na machapisho mbalimbali yanayohusu muundo wa kirai kitenzi katika lahaja mbalimbali kama vile Kitumbatu na Kimakunduchi. Lahaja hizi zimerejewa ili kuonyesha muundo wa kirai kitenzi katika lugha nyengine zinazokaribiana na Kiswahili au zile za jamii yake ambazo ni lugha za Kibantu. Sehemu ya pili ya sura hii imeelezea kiunzi cha nadharia kilichotumika katika utafiti huu.

2.2 Mapitio na Machapisho

Katika sura hii utafiti utaangalia mambo yafuatayo ;

Tafiti zinazohusu Kitumbatu, machapisho katika Kiswahili Sanifu, kiunzi cha nadharia kilichotumika katika utafiti huu na hitimisho.

2.3 Tafiti zinazohusu Kitumbatu

Kama ilivyoelezwa kwenye sura ya kwanza, utafiti japo mdogo umefanywa kuhusu lahaja ya Kitumbatu. Matokeo ya utafiti huo yametoa maelezo machache ambayo yana mchango kiasi katika ulimwengu wa isimu na lugha ya Kiswahili kwa ujumla. Baadhi ya waliofanya utafiti kuhusu Kitumbatu ni:

Stigand (1915) akinukuliwa na Makame (2012), ameandika kuhusu mabadiliko ya kisarufi katika lahaja za Kiswahili akidai kuwa lahaja hizo zimegawika katika makundi kumi na matano. Makundi hayo anayataja kuwa ni kundi la Zanzibar lenye

lahaja kuu za Kiunguja, Kimrima, na Kimgao, lahaja ndogo za Zanzibar ni Kitumbatu, Kihadimu na Kipemba. Katika kazi yake hii ameeleza mabadiliko katika lahaja za Kimvita, Kimgao na Kiunguja. Mabadiiko aliyoyaonesha ni pamoja na mabadiliko ya sauti, mabadiiko ya sarufi, mabadiliko ya msamiati na mabadiiko ya nahau. Kwa mfano, kuhusu mabadiliko kaika sauti baina ya Kiunguja na Kimvita, anaeleza kuwa [ch] au fonimu /ʃ/ katika Kiunguja huwa sauti [t] au fonimu / t/ katika Kimvita na sauti [j] au fonimu /*ƒ* / katika Kiunguja huwa sauti [d] au fonimu /d/ katika Kimvita, kama inavyoonekana kwenye mfano nambari 1 ufuatao hapa chini.

a)	[tʃ] Kiunguja	[t] Kimvita
	Mchanga	Mtanga
	Macho	Mato
b)	[*ƒ*] njaa	[d]ndaa
	Nje	Nde

Mifano nambari 1 inaonesha mabadiliko ya sauti katika lahaja ya Kiunguja na Kimvita. Lakini hakutueleza mabadiliko yoyote ya lahaja yaliyomo katika Kitumbatu. Ameeleza tu kuwa Kitumbatu ni lahaja inayopatikana Kaskazini mwa Kisiwa cha Unguja, Zanzibar na kuwa Kihadimu ni lahaja ya Mashariki na kusini ya Kisiwa cha Zanzibar. Pamoja na Stigand (1915) kueleza mambo mbali mbali kuhusu lahaja ya Kitumbatu, hata hivyo hakueleza chochote kuhusu mabadiliko ya kisarufi yaliyomo katika lahaja ya Kitumbatu wala miundo yake.

Vilevile Makame (2012) akimnukuu Hill (1973) anasema kuwa alifanya utafiti katika Kitumbatuna Kimakunduchi kwa kuangalia sauti zilizomo ndani ya lahaja hizo Aliangalia sauti [o], [t], [c], na [k] ili kuona msambao wa sauti hizo katika lahaja

nyingine tisa kama Chifundi, Kiamu, Kijomvi, Kimiini, Kimtangata, Kimvita, Kipemba, Kiunguja, Kisiu na Kitikuu. Utafiti huu pia haukueleza muundo wa kisarufi katika Kitumbatu.

Maganga (1991) akinukuliwa naMakame (2012) alisema kuwa alifanya utafiti juu ya mofofonolojia katika lahaja za Kiswahili akilinganisha maumbo hayo katika lahaja za Kitumbatu, Kipemba, Kimakunduchi na Kiswahili sanifu. Katika utafiti wa Maganga, lahaja ya Kitumbatu ililinganishwa na lahaja nyingine katika kipengele cha mofofonolojia ambapo masuala kama ya tangamano la irabu yaliangaliwa hadi katika ngazi ya aina za maneno kama vile nomino, vitenzi na kadhalika.Utafiti huo, umeonesha tangamano la irabu linavyotokea katika lahaja ya Kitumbatu . Kwa mfano, wakati viambishi vya nafsi vinapokutana na mzizi wa kitenzi unaoanza na irabu, matokeo huwa kama inavyoonekana kwenye mfano nambari 2 ufuatao:

	Kitumbatu	**Kiswahili sanifu**
A	Nyambia (ni+ambie)	Niambie
B	Weze (u+eze)	Utafute
C	Etwe (a+itwe)	Aitwe
D	Ende (a+ende)	Aende
E	Tone (tu+one)	Tuone

Mifano nambari 2 inaonesha irabu katika viambishi nafsi hubadilika kwa namna mbalimbali au kudondoshwa kabisa. Hivyo, utafiti huu ni muhimu sana kwani utasaidia kupata vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu na jinsi vinavyokuwa vikilinganishwa na Kiswahili sanifu.

Mwingine aliyeandika juu ya lahaja mbalimbali za Kiswahili,Kitumbatu ikiwa ni mojawapo ni Kipacha (2003) .Katika kazi yake amejaribu kuonesha matini za Kitumbatu zikiwemo mashairi na hadithi. Vilevile ameonesha orodha ya leksimu za Kitumbatu zinavyotofautiana na zile za Kiswahili sanifu (Kipacha 2003; 145) kama ifuatavyo:

Namb	**Kitumbatu**	**Kiswahili sanifu**
A	Kiza	Giza
B	Gino	Jino
C	Pakusa	Pangusa
D	Gani	Jani

Katika mifano hii tunaona kuwa sauti [g] katika Kitumbatu hubadilika na kuwa [ʤ] katika Kiswahili sanifu.Stude (1995) ni mtaalamu mwingine aliyenukuliwa na Makame (2012) ambaye alifanya utafiti katika lahaja ya Kitumbatu kwa kuangalia urekebishaji na mabadiliko ya lugha katika Kitumbatu. Aliangalia tofauti za sauti kati ya Kitumbatu na Kiswahili sanifu na kuelezea kuwa Kitumbatu kina sauti [l*] inayotamkwa pamoja na irabu inayofuatana nayo na kuipa sauti hii sifa ya vokali. Sauti hii haipatikani katika Kiswahili sanifu. Pia ameonesha mabadiliko ya sauti na tofauti ya msamiati katika Kitumbatu na Kiswahili sanifu na aliingiza baadhi ya mifano kutoka katika lahaja ya Kimakuduchi. Kwa mfano sauti [l] inayokaa mwazoni mwa neno katika Kitumbatu hujitokeza kama /j/ katika Kimakunduchi na hujitokeza kama /u/ katika baadhi ya maneno ya Kiswahili sanifu. Lakini [v] kama vumbi kwenye Kiswhili sanifu huwa [d]katika Kitumbatu, neno lala hutafautika kimatamshi kwani Kitumbatu hutumia /l'/ yenye uvokali na hutamkwa /l'al'a/ .Sauti [y] au fonimu /j/ huoneshwa pia katika Kimakunduchi.

Tuangalie mifano hii kama ifuatavyo.

Namb	**Kitumbatu**	**Kimakunduchi**	**Kiswahili sanifu**
A	L'umia	Yumia	Umia
B	L'umiza	Yumiza	Umiza
C	L'omba	Yomba	Omba
D	L'al'a	Yaya	Lala

Mifano hii huonesha maneno yanayoanza na sauti [l] katika Kitumbatu yanaanza na irabu katika Kiswahili Sanifu. Kama wataalamu wengine ambao kazi zao tumezijadili Stude (1995) naye hakuangalia miundo ya kisarufi katika Kitumbatu ukiwemo wa virai tenzi.

Wengine waliochangia ni BAKIZA (2012) wao pamoja na kutoa maana za maneno kwa lahaja ya Kitumbatu pia wametoa tafauti ya sarufi ya Kitumbatu na sarufi ya Kiswahili. Sarufi ya lahaja ya Kitumbatu inafanana na sarufi ya Kiswahili sanifu, ingawa matamshi yanayotafautiana.

Mfano katika viwakilishi vya nafsi Kama ifuatavyo:

Nafsi	**Kiswahili sanifu**	**Kitumbatu**
Nafsi ya 1 umoja	Mimi ninakuja	Miye sakuja
Nafsi ya 1 wingi	Sisi tutakuja	Suye tuchakuja
Nafsi ya 2 umoja	Wewe utakuja	Weye kuchakuja
Nafsi ya 2 wingi	Nyinyi mtakuja	Nyuye mchakuja
Nafsi ya 3 umoja	Yeye atakuja	Veye kachakuja
Nafsi ya 3 wingi	Wao watakuja	Veo wachakuja

Machapisho yanayohusu tafiti za Kitumbatuliyopita yalitusaidia katika utafiti wetu ijapokuwa hakukua na utafiti wowote uliofanyika kuhusu kipashio kirai kitenzi katika Kitumbatu.Machapisho hayo yalitusaidia kuweza kujua tungo za lahaja ya Kitumbatu zinavyojengwa kwa kutumia vipashio mbalmbali. Hivyo mapitio yanayofuata yalihusu zaidi kuhusu kipashio hicho katika lugha zinazokaribiana na Kiswahili au zile za jamii yake.

2.2.2 Machapisho Katika Kiswahili Sanifu

Massamba na wenzake (2009) wameeleza kuwa kirai kitenzi ni kirai ambacho kimekitwa katika kitenzi au katika mahusiano ya kitenzi na neno au mafungu mengine ya maneno, na neno kuu katika aina hii ya kirai huwa ni kitenzi. Wao wamesema katika lugha ya Kiswahili kuna miundo ya kirai kitenzi ifuatayo:

a) Kitenzi peke yake

   Mfano: amekufa,

b) Kitenzi na nomino moja

   Mfano: ameandika barua

c) Kitenzi na nomino mbili

   Mfano: amempa mtoto chakula

d) Kitenzi na kitenzi

   Mfano: anapenda kusoma

e) Kitenzi na nomino na kitenzi

   Mfano: anamfundisha mtoto kusoma

f) Kitenzi (na kwamba /kuwa)na sentensi

   Mfano: amesema (kwamba) atarudi kesho.

g) Kitenzi na nomino (na kwamba /kuwa) na sentensi

Mfano: amemwagiza mama (kwamba) aniletee chumvi.

Kwa mujibu wa Matinde (2012), muundo wa kirai kitenzi ni pamoja na

a) Kitenzi kimoja

Mfano: tumefika

b) Kitenzi na nomino moja

Mfano: wamenunua viatu

c) Kitenzi na nomino mbili

Mfano: amempa mtoto zawadi

d) Kitenzi na kitenzi

Mfano: anapenda kucheza

e) Kitenzi na kielezi

Mfano: ameenda shuleni

f) Kitenzi, nomino na kitenzi

Mfano: tunawataka viongozi kuwajibika

Wataalamu wengine waliozungumzia kirai kitenzi ni Masebo na Nyangwine (2007) ambao wameeleza kuwa kuna miundo ya kirai kitenzi ifuatayo;

a) Kitenzi peke yake

Mfano: Tutapigana

b) Kitenzi na nomino moja

Mfano: Tumesomewa risala

c) Kitenzi na nomino mbili

Mfano: Wamempigia Juma kelele

d) Kitenzi na kitenzi

Mfano: Tunataka kulala

e) Kitenzi, nomino na kitenzi

Mfano: Tuliwataka viongozi kututembeleaKitenzi na kivumishi

f) Kitenzi na kivumishi

Mfano: Ni mzuri

g) Kitenzi na kirai kiunganishi

Mfano: Alikuwa na pesa

h) Kitenzi na nomino pahala

Mfano: Yumo darasani

i) Kitenzi na kielezi na kitenzi

Mfano: itakuwa vizuri kumtembelea

Machapisho ya mapitio haya yamesaidia sana kwa kuweka wazi kuwa muundo wa kirai kitenzi katika Kiswahili sanifu unafanana na ule muundo wa kirai kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu kwa mpangilio wake wa vipashio katika uundaji wa tungo.

2.4 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti huu ulitumia nadharia ya Sarufi Jumuishi ya Miundo Virai (*Generalised Phrase Structur*e *Grammar)*. Hii ni moja wapo ya nadharia za Sarufi Miundo Virai zinazotumika kuelezea sintaksia ya lugha, nadharia hii ilianzishwa na Gerald Gazdar mwaka(1970). Wataalamu wengine wa isimu kama Ivan Sag, Ewan Klein na Geoffrey Pullun walitoa mchango wao katika nadharia hii katika kitabu cha *Generalized Phrase StructureGrammar* walichoandika pamoja na Gazdar (1985). Nadharia hii

inatafautiana na nadharia ya Sarufi Zalishi kwa kushughulikia kiwango kimoja cha kimuundo ambacho ni umbo la nje (Gazdar na wenzake 1985; 10) .Hivyo nadharia hii haiangalii umbo la ndani la kipashio kama ilivyo katika nadharia ya Choamsky ya Sarufi Zalishi. Umbo la nje ni ule muonekano halisi wa muudo wa kipashio (Kihore 1994 ; 12) Pia nadharia hii inahusu kiwango kimoja cha sarufi, yaani sintaksia.

Nadharia ya sarufi Jumuishi ya Miundo Virai inazingatia kanuni inayoruhusu kuwepo kwa mti wa matawi ya kisintaksia. Kanuni hii ni kanuni ya utawaliwa wa moja kwa moja (Immediate Dominance Rule). Katika mchoro huu kila kifundo mbali na mzizi kina uhusiano wa udada:



Au A ⟶ B, C, D

Katika mchoro huu kielelezo hicho A ndio mama wa vifundo B, C na D na vina uhusiano wa udada. Katika nadharia hii mzizi mama ni kirai na dada ni kipashio kikuu na vijalizo vyake. Kwa mfano wa tungo ifuatayo: “amemletea mtoto chakula”, Tungo hiyo ni kirai kitenzi katika lugha ya Kiswahili ambapo KT ni A ambao ndio mzizi mama, kitenzi ‘amemletea’ ni B, neno “mtoto” ni C na, neno “chakula ni D. Vipashio vyote hivyo vina uhusiano wa udada kwani kila kimoja kinatoa taarifa kwa mwenzake. Pia katika mchoro huo kuna uhusiano wa utawala na utangulizani ambapo B ni kitenzi ambacho kimetangulia vipashio vyingine vyote vilivyomo kwenye tungo hiyo. Katika nadharia hii kirai kitenzi kimeainishwa kwa sifa mbalimbali kama ifuatavyo:

1. KT - T(1)

   Mfano " ruins"

2. KT - T(2) KN

   Mfano KT "sing the song"

3. KT - T (3), KN, KH (to)

   Mfano "give the scissors to sandy"

4. KT - T (4), KN, KH (for)

   Mfano "bought a record for lee"

5. KT - T (5), KN, KN

   Mfano "hand Kim the Onions"

6. KT - T (6), KN, KH (mahali)

   Mfano "put the magazines in the rack

7. KT chenye kitenzi kisaidizi - T (7), KE

   Mfano "is standing in the garden"

Ufunguo

KT kirai kitenzi

KN kirai nomino

KH kirai kihusishi

KE kirai kielezi

Vitenzi hivyo vimeainishwa kwa namba kulingana na vipashio vinavyoandamana na kitenzi husika. Kama ilivyoonyeshwa, kirai kitenzi chenye kitenzi kimoja, kitenzi hicho kimepewa sifa ya nambari moja (1) na chenye kitenzi na kirai nomino kitenzi kimepewa nambari mbili (2) na kadhalika.

Hivyo, katika utafiti huu mtafiti alichambua kirai kitenzi katika lahaja ya Kitumbatu kwa kutumia nadharia ya Sarufi Jumuishi ya Muundo Virai. Mtafiti amechagua nadharia hii kwasababu ni nadharia ambayo inajihusisha na kiwa ngo kimoja tu cha kisarufi ambacho ni sintaksia. Vilevile ni nadharia ambayo inaangalia kiwango cha kimuundo ambacho ni umbo la nje tu ambapo ni tafauti na nadharia nyengine.

Mtafiti mwengine aliyewahikutumia nadharia hii katika utafiti wake ni Masoud (2011) ambaye alifanya utafiti kuhusu muundo wa virai vitenzi katika lugha ya Kisambaa.Nadharia hii inafaa kuliko nadharia nyengine kwasababu hii haiangalii vitu vingi kama Nadharia ya Sarufi Zalishi ya Choamsky ambayo inaangalia umbo la ndani na la nje.

Nadharia hii ilitumika kuchambua malengo ya utafiti huu kwa kuonesha miundo ya kirai kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu na sentensi zake ambapo nadharia hii huonesha uhusiano wa kila kipashio, kwa vile nadharia hii imejikita zaidi na uchanganuzi wa miundo ya virai kwa kuonesha umbo la nje la kirai husika.

Nadharia hii ilichambua lengo la kwanza kwa kuonesha vipashio ambavyo vinafuatana na kirai kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu.Lengo la pili na la tatu lilichambuliwa kwa kuonesha jinsi sentensi za lahaja ya Kitumba zinavyokuwa , pamoja na kuonesha kuwa vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu vinaweza kuwa ni elekezi au sio elekezi kutokana na kuwa nadharia hii inaangalia umbo la nje tu.

2.3 Hitimisho

Kwa ujumla sura hii imeelezea mapitio na mchapisho ya tafiti zinazohusu Kitumbatu na machapishokutoka kiswahili sanifu. Vile vile sura hii imeeleza kiunzi cha nadharia.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii itajadili mbinu za utafiti zitazotumika katika utafiti ambapo inaeleza mahali pa utafiti, watoa taarifa, sampuli iliyotumika, mbinu za ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na vifaa au zana zilizotumika katika utafiti huu.

3.2 Eneo la Utafiti

Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inajumuisha Visiwa viwili vikubwa ambavyo ni Unguja na Pemba – na zaidi ya visiwa vidogo 14 (RGoZ, 1992) ambavyo vyingine vinakaliwa na watu na vyengine havikaliwi na watu. Unguja ipo wastani wa kilomita 40 kutoka Tanzania Bara na Pemba ni kilomita 60. Miongoni mwa visiwa vidogo dogo vinavyokaliwa na watu ni Kisiwa cha Tumbatu. Utafiti huu umefanyika katika Kisiwa hicho ambacho ni eneo halisi la wazungumzaji wa lahaja hii. Kisiwa hiki kipo katika Kisiwa cha Unguja, Wilaya ya Kaskazini 'A', Mkoa wa Kaskazini Unguja na kipo umbali wa kilomita 48 kutoka Mjini Unguja na kilomita 3 kutoka Mkokotoni, kina urefu wa kilomita 15.5 na upana wa kilomita 2.5.

Wakaazi wanaoishi katika Kisiwa hiki wanajishughulisha sana na kazi ya uvuvi na kilimo kuliko ufugaji. Hii ni kutokana na maumbile ya kijografia ya Kisiwa hiki. Kisiwa hiki kimegawika katika maeneo mawili makubwa ambayo ni Jongowe na Kichangani. Jongowe ipo upande wa Kusini mwa Kisiwa na Kichangani ipo upande wa Kaskazini. Wenyeji wa kisiwa hiki wanaitwa Watumbatu.

3.3 Sampuli ya Utafiti

Katika utafiti watoa taarifa ni watu, makundi ya watu, na katika tafiti nyingine huwa ni vitu na viumbe hai vingine. Katika utafiti huu watoa taarifa walikuwa ni baadhi ya wakaazi wa Kisiwa cha Tumbatu ambao ni watumiaji wa asili wa lahaja hii, wakaazi hawa walipatikana katika eneo la Jongowe na Kichangani ambayo ndio maeneo makubwa ya Kisiwa cha Tumbatu. Watoa taarifa walikuwa ni watu wazima wenye umri kuanzia miaka 70 na kuendelea ambao ni wanawake na wanaume. Aidha, utafiti haukuhusisha kundi la vijana kwa sababu tayari lahaja ya Kitumbatu kwa kundi hili imeshaathiriwa na Kiswahili sanifu na badala yake uliwahusu wazee tu ambao ni wazawa wa Kisiwa cha Tumbatu ambao hawajaathiriwa na Kiswahili sanifu. Kundi hili la wazee limechaguliwa kwa kuwa bado linazungumza lahaja ya Kitumbatu asilia na hivyo, limeweza kutoa data za usahihi, kwani ndio watu ambao wanaifahamu ipasavyo lahaja ya Kitumbatu. Watoa taarifa walichaguliwa kwa vigezo maalum vya umri na jinsia kutoka katika vijiji hivyo. Hivyo, jumla ya watoa taarifa 25 walichaguliwa, kati ya hao 10 walikuwa ni wanaume na 15 ni wanawake.

Katika utafiti huu idadi ya wanawake ilikuwa ni kubwa kuliko wanaume kwasababu idadi ya wanaume wenye umri kuanzia miaka 70 ni ndogo ukilinganisha na idadi ya wanawake wenye umri kama huo. Data zilizotolewa na watu hao ndizo zilizotumika kufanya uchambuzi wa miundo mbali mbali ya kirai kitenzi katika lahaja ya Kitumbatu.

3.4 Uteuzi wa Sampuli

Kwa mujibu wa Kothari (1990) sampuli ni idadi au kundi dogo lililochaguliwa kuwakilisha sifa za kundi kubwa kutoa majumuisho ya data zilizokusanywa. Sampuli

inaweza kuwa ni watu, elementi na majengo yaliyoteuliwa kwa niaba ya watu wote. Utafiti huu umetumia sampuli kusudio ambayo ni aina ya usampulishaji ambayo utafiti huchagua sampuli kulingana na malengo maalum. Kwa mujibu wa Mlyuka (2011) kama ilivyoelezwa na Kothari (2004) kuwa uzuri wa utafiti ni kwa mtafiti kuchagua watoa taarifa wanaofaa kwa utafiti wake.

Utafiti huu ulihusisha watafitiwa 25 wakiwemo wanawake (15) na wanaume (10) kutoka maeneo ya utafiti ambayo ni Kijiji cha Jongowe na Kijiji cha Gomani. Utafiti ulichagua idadi ya watafitiwa 25 kwasababu ni idadi ya yenye uwakilishi yenye kukidhi katika kutoa taswira yenye kujitosheleza ya wahusika kwa ajili ya kueleza hali halisi ya malengo ya utafiti. Kwa ujumla watafitiwa wote walikuwa kwenye umri kuanzia miaka70 nakuendelea. Watafitiwa wa utafiti huu walikuwa ni wenye elimu ya chini ambayo iliwasaidia kujua kusoma na kuandika tu. Vigezo vilivyotumika kuwapata watafitiwa hawa ni umri na makaazi yao ya kudumu ambapo kutokana na utafiti huu walihitajika wakaazi halisi wa Tumbatu ambao wanazungumza na kukijua Kitumbatu kiundani bila ya kuchanganya na Kiswahili sanifu na ndio waliotoa taarifa zote za utafiti huu. Mgawanyo wa Watafitiwa kwa mujibu wa vijiji wanavyotoka ni kama ifuatavyo :

ENEO	**IDADI YA WATAFITIWA**		**JUMLA**
	Wanaume	Wanawake	
Jongowe	5	8	13
Kichangani	5	7	12
Jumla	**10**	**15**	**25**

Sampuli kusudio ilisaidia kupata watoa taarifa wanaotakiwa ili kupata taarifa sahihi. Aidha, uteuzi huu wa sampuli ulizingatia zaidi wazawa wa Kisiwa cha Tumbatu kwasababu ndio wenye data za asili na za uhakika kutokana na kuwa wanauelewa mzuri na lahaja hiyo. Kama inavyofahamika kuwa umuhimu wa sampuli unategemea tabia mbalimbali za mada inayoshughulikiwa. Ikiwa mada ina mawanda makubwa au ina tabia mbalinbali basi sampuli huwa kubwa. Lakini mada ikiwa imejikita katika tabia moja sampuli inayochaguliwa inatakiwa iwe na ufanisi. Kutokana na hali hiyo muundo wa virai-tenzi katika lugha uaonekana kuwa ni wa tabia funge kuliko mada inayohusu tabia za watu. Hivyo basi, mtafiti ameridhika kuwa sampuli ya watu ishirini na tano itakuwa na ufanisi katika utafiti wake.

3.5 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu ulitumia mbinu ya hojaji (dodoso) katika ukusanyaji data ili kupata taarifa sahihi: Kuna wataalamu kama (Goods & Hatt 1959) wanaeleza kuwa hojaji ni seti ya maswali yaliyoandikwa au kauli zinazohusiana na suala linalotafitiwa ambayo mtafiti hutoa kwa wasailiwa kwa ajili ya kuibua habari, majibu, maoni, mitazamo na mikabala mahsusi kuhusu mada ya utafiti. Kothari (2004) amesema kuwa dodoso ni mbinu ya utafiti ambayo mtafiti anaandaa maswali yake yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani. Maswali hayo yanaweza kuhitaji majibu mafupi au marefu kutegemea taarifa inayohitajika na mtu anayepewa dodoso hizo. Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti kukusanya data ambazo zimetoka kwa wazawa wa lahaja yenyewe.

Utafiti huu ulitumia njia hii kwa kuwa taarifa husika za utafiti zilipatikana moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa,mtafiti alitumia hojaji ili kupata taarifa kutoka kwa watoa taarifa. Hojaji zimetayarishwa zikiwa na maswali yaliyogawiwa sehemu tatu, sehemu

ya kwanza ilihusiana na maelezo binafsi ya mtafitiwa ambayo ilikuwa na maswali sita (6), sehemu ya pili ilikuwa na maswali ambayo mtafitiwa alitakiwa kubadilisha sentensi za Kiswahili sanifu kwenda lahaja ya Kitumbatu ambapo sehemu hii ilikuwa na jumla ya maswali thalathini na matano (35) na sehemu ya tatu mtafiti alitakiwa kubadilisha sentensi za lahaja ya Kitumbatu kwenda Kiswahili sanifu na jumla ya maswali thalathini na matano (35) yaliorodheshwa katika sehemu hii ambapo kwa ujumla hojaji hii ilikuwa na maswali sabini na sita (76). Mtafiti alikwenda na hojaji hizo kwa watoa taarifa na alitoa karatasi zenye maswali ili watoa taarifa waweze kuzijaza. Watoa taarifa pia walitakiwa kushauri na kueleza miundo mingine ya virai wanayoijua ambayo haikuorodheshwa kwenye hojaji ambayo watoa taarifa wanaielewa na wanaweza kuieleza kwa kutumia mifano wanayoijua.

Mbinu hii ya utafiti ilijitosheleza na kukamilisha utafiti huu kwa sababu mtafiti alitoa karatasi zenye dodoso na kuwapa watafitiwa ili watoe taarifa na data zenye uhakika. Hii ilisaidia kupata taarifa sahihi kutoka kwa walengwa husika ambao ni wazawa na wazungumzaji wa lahaja ya Kitumbatu.

3.6 Faida na Hasara za Mbinu ya Hojaji ama Dodoso

3.6.1 Faida Faida kubwa za Mbinu Hii ya Hojaji Ama Dodoso niPamoja na:

(a) Mbinu hii haina upendeleo wowote kwasababu maswali yote yanakuwa sawa.

(b) Maswali yanayotumika katika mbinu hii huandaliwa vizuri tangu mwanzo.

(c) Majibu yanatokana na mtu mmoja tu yule anayejibu.

(d) Inaweza kutumia sampuli kubwa.

(e) e) Mtoa taarifa anaweza kujaza dodoso kwa wakati ambao atakuwa na nafasi nzuri zaidi ya kujaza.

Hasara za mbinu hii

Hasara kubwa zinazoweza kujitokeza kwenye mbinu hii ni:

(a) Zinaweza dodoso zisijibiwe na wala zisirudishwe

(b) Dodoso zinakuwa na udhibiti mdogo na nyengine kupotea kabisa.

(c) Ni vigumu kujua kama hao waliojibu ndio wawakilishi hasa waliokusudiwa.

Hasara hizo zimedhibitiwa kwa kuhakisha kuwa wanaojaza ndio hasa waliokusudiwa na kulikuwa na ufuatiliaji mzuri kwa watoa taarifa wote.

3.7 Uchanganuzi wa Data

Mtafiti alitumia mkabala stahilifu katika uchanganuzi wa data ambao ni ule unaotumia maelezo katika kuchanganua data. Mkabala huu wa uchanganuzi umechaguliwa kwa sababu data zitakazokusanywa zilikuwa katika hali ya maelezo. Pia lengo la ufatiti huu ni kuonyesha muundo wa kirai kitenzi ambao utajibainisha vizuri zaidi utakapoelezwa kwa kutumia maelezo. Hivyo, data zote zilizopatikana zilichambuliwa kwa njia ya maelezo kwa ajili ua kufikia lengo la utafiti huu.

3.8 Hitimisho

Kwa ujumla sura hii imejadili vipengele vya mahali pa utafiti, sampuli ya utafiti, sampuli iliyotumika, mbinu za ukusanyaji taarifa, uchanganuzi wa taarifa pamoja na vifaa au zana zilizotumika katika utafiti huu.Sura ya nne inahusiana na uwasilishaji na uchmbuzi wa data.

SURA YA NNE

UWASLISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Utafiti huu umeweza kutumia njia ambayo imeelezwa hapo juu, ambayo ni kutumia mbinu ya dodoso kwa watafitiwa ambao ni wazungumzaji wa lahaja yaKtumbatu. Kwa kutumia dodoso hizo utafiti umeweza kukusanya sentensi sabini ambazo zilipatikana kwa watafitiwa. Sentensi za lahaja ya Kitumbatu ziliorodheshwa na kufanyiwa uchambuzi. Dodoso ziliandaliwa na kuchambuliwa ili kurahisisha kujibu maswali matatu ya utafiti huu kwa dhamira ya kufikia kwenye malengo mahususi na lengo kuu la Utafiti huu. Hivyo, uchambuzi wa taarifa za utafiti huu umefanywa kwa kuangalia mambo yafuatayo:

(i) Kirai kitenzi cha Kitumbatu kina muundo gani na vipashio gani vinaandamana nacho?

(ii) Sentensi za lahaja ya Kitumbatu zinamuundo gani?

(iii) Uelekezi katika vitenzi vya lahaja ya kitumbatu unajitokezaje?

4.2 Matokeo ya Utafiti

4.2.1 Muundo na Vipashio wa Kirai Kitenzi cha Lahaja ya Kitumbatu

Kirai kitenzi ni kirai ambacho huundwa kwa kitenzi na maneno mengine yanayohusiana na kitenzi hicho (Matinde 2012). Neno kuu katika kirai hiki ni kitenzi chenyewe. Vipashio vinavyoweza kufuatia kitenzi ni nomino, vielezi, sentensi na vihusishi. Vitenzi ambavyo lazima vifuatiwe na nomino huitwa vielekezi na

visivyofuatiwa na nomino huitwa visivyoelekezi. Utafiti huu umegundua kuwa katika lahaja ya Kitumbatu kuna miundo ya kirai kitenzi ya aina nane (8) ifuatayo:

Kirai kitenzi chenye kitenzi pekee

Hiki ni kirai kitenzi ambacho huundwa na kitenzi pekee. Mifano ya kirai kitenzi chenye kitenzi pekee vilivyotolewa na watoa taarifa ni:

Kirai kitenzi chenye kitenzi pekee (lahaja ya Kitumbatu)	**Kiswahili Sanifu**
Tuchamchuza	Tutamuangalia
Kaja	Amekuja
Kankokeza	Ananyonyesha
Kafu	Amekufa
Wanauka	Wanaondoka

Katika mifano ya hapo juu inaonesha kuwa kirai kitenzi cha lahaja ya kitumbatu kinaweza kuundwa na kitenzi pekee. Mchanganuo wa hapo chini uliofanywa kwa kutumia mchoro unaonesha muundo wa kirai kitenzi chenye kipashio kimoja tu ambacho ni kitenzi. Hali hii imejidhihirisha kutokana na muundo wa mchoro kuwa na tawi moja tu. Pia mchoro huo unatuonesha pia kuwa hicho kipashio kimoja kilichowekwa ni kitenzi.

Kirai kitenzi naNomino Moja

Hiki ni kirai kitenzi ambacho huundwa na kitenzi na nomino ambapo nomino zinaweza kuwa ni majina ya watu kama Asha, Juma, au Mboja. Pia nomino zinaweza kuwa majina ya wanyama kama simba, Chui na Kuku na majina ya kawaida kama samaki, kalamu, mkono nakadhalika. Mifano ya aina ya kirai kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu ambayo imetajwa na watoa taarifa ni pamoja na:

Kirai kitenzi na nomino moja (lahaja ya Kitumbatu)	**Kiswahili Sanifu**
Kagele simu	Amepoteza simu
Kachukuu kuku	Amechukua kukua
Wancheza mpira	Wanacheza mpira
Kamgwili mwivi	Amemkamata mwizi
Wankulya ubwabwa.	Wanakula wali

Mfanowa mchoro wenye kirai kitenzi na nomino moja ni:

Kanjiki mhogo:



Virai vitenzi vilivyooneshwa hapo juu vinaonekana kuundwa na kitenzi pamoja na kirai nomino ambacho kinaundwa na nomino moja tu. Vipashio hivyo vinavyounda kirai kitenzi chenye kitenzi na nomino moja vina uhusiano wa utawalia na utangulizani. Katika uhusiano huo kirai kitenzi kinatawala kitenzi na nomino wakati kitenzi kinatangulia nomino. Kitenzi hicho kinapoandamanana nomino ndipo kinapata sifa ya uelekezi. Nomino hizo ndizo zinazoleta ukamilifu wa maana katika tungo husika.

Kirai Kiitenzi Chenye Kitenzi naNominoMbili

Kirai hicho ni kile chenye kitenzi elekezi ambacho kinakuwa ni nomino mbili. Nomino hizo ndizo zinazoleta ukamilifu wa maana husika katika tungo husika. Mfano wa kirai hiki ni:

Kirai kitenzi chenye kitenzi na nomino mbili (lahaja ya Kitumbatu)	**Kiswahili Sanifu**
Wamki mwana zawadi	Wamempa mtoto zawadi
Kamnunulili mwanafunzi kalamu	Amemnunulia mwanafunzi kalamu
Kachampikia ubwabwa mtoto	Atampikia mtoto wali
Kamfanyili mwalimu zogo	Amemfanyia zogo mwalim
Dakitari kamtoogo mgonjwa shindano	Daktari amemchoma mgonjwa sindano

Aidha, mchoro ufuatao unatoa ufafanuzi wa kirai kitenzi chenye kitenzi na nomino mbili:



Kirai Kitenzi Chenye Kitenzi na Kitenzi au Vitenzi Viwili

Muundo wa kirai kitenzi cha aina hii unakuwa na kitenzi kikuu kimoja na kitenzi kisaidizi kimoja. Kitenzi kisaidizi ni kitenzi kinachosaidia kitenzi kikuu ili kuleta maana kamilifu (Matinde, 2012). Kitenzi hiki huambatana na kitenzi kikuu ambacho kikawaida hudokeza muda ambao tendo limefanyika au litafanyika. Aidha, kitenzi hiki hutumika katika kudhihirisha uyakinifu au ukanushi wa kitendo (Matinde, 2012).

Kitenzi kisaidizi kina sifa ya kusaidia kitenzi kikuu ili sentensi ilete maana kamili kwa wakati unaotakiwa. Kitenzi kisaidizi huwakilishwa kwa (Ts). Kitenzi kikuu hutangulia na kitenzi kisaidizi hufuatia. Mifano wa vitenzi visaidizi kwa lugha ya Kiswahili sanifu ni alikuwa, ataweza, alikwenda, anaendelea, anataka, anapenda nakadhalika. Mifano ya vitenzi visaidizi vya lahaja ya Kitumbatu ni:

Kitumbatu	**Kiswahili Sanifu**
Kavu	Alikuwa

Katavyeza	Ataweza
Kantaka	Anataka
Kanpenda	Anapenda

Mifano ya tungo yenye kirai hicho ni hii ifuatayo:

Kitumbatu	**Kiswahili Sanifu**
Twantaka kulya	tunataka kula
Katavyeza soma	ataweza kusoma
Wanpenda kwandika	wanapenda kuandika
Nivu halima	tuvu tukacheza
Nilikuwa nikilima	tulikuwa tukicheza

Mfano wa kirai kitenzi chenye vitenzi viwili ni:

Kavu akoga - alikuwa anakoga



Virai vilivyooneshwa hapo juu vinaonekana kuundwa na kitenzi kisaidizi na kitenzi kikuu ambapo kitenzi kikuu kinatanguliwa na kitenzi kisaidizi ambapo kitenzi

kisaidizi kikikaa peke yake hakiwezi kutoa maana kamilifu ya sentensi lazima kifuatane na kitenzi kikuu. Kwa mujibu wa Masoud (2011) anasema kuwa katika lugha ya Kiingereza vitenzi visaidizi vinafanya kazi mbali mbali kama vile kuonyesha hali ya kuendelea tendo hali ya utimilifu, kuonyesha msisitizo wa jambo, hali ya mzungumzaji na kauli ya kutendwa.

Dhima za vitenzi visaidizi katika lugha ya Kiingereza inakuwa kama ifuatavyo :

Kitenzi	**Dhima**	**Sentensi**
Am	Kuendelea	Iam reading a book
Was	Kutendwa	Iwas born in 1990
May	Mzungumzaji	You may do
Do	Msisitizo	I do like this shoes
Have	Halitimilifu	You have finished to wash

Katika lahaja ya Kitumbatu mfuatano wa tungo kama huo pia upo. Kufuatana huko kunahusu ulazima wa kuwepo kitenzi kikuu pamoja na kitenzi kisaidizi ili kuwa na ukamilifu wa kimatumizi wa tungo hizo.

Kirai kitenzi Chenye Kitenzi, Kishazi Tegemezi/ Kishazi Kijalizi na Sentensi

Kirai kitenzi cha aina hii ni kirai ambacho kinaundwa na kijalizi tegemezi ambacho kinaunganisha vipashio vyenye utegemezi, kishazi kijalizi hicho ni kuwa aukwamba**.** Katika lahaja ya Kitumbatu kirai hiki kinajaliza kitenzi ambacho kinategemea kikamilishwe na sentensi. Katika Kiswahili sanifu kuna tungo kama:

"Mtoto amelalamika kwamba amelazimishwa kwenda shule"

Katika tungo hii kuna kirai kitenzi amelalamika, hivyo kishazi tegemezi 'kwamba' kimeweza kuunganisha kirai kitenzi amelalamika na sentensi amelazimishwa kwenda shule kutokana na udhihirishwaji wa kishazi hicho. Katika lahaja ya Kitumbatu pia kuna tungo au sentensi zenye muundo wa aina hiyo; mfano:

Baba kaseme kwamba kan'ndaMjini –Babaamesema kwamba anakwendamjini.Hivyo basi, kutokana na kuwepo sentensi za aina hiyo katika lahaja ya Kitumbatu inadhihirisha kuwepo kirai kitenzi chenye muundo wa kitenzi, kishazi tegemezi na sentensi. Mifano mengine ya Virai hivyo ni kama ifuatavyo:

- Baba kaseme kuwa hanrudi nyumbani - baba amesema kuwa hatarudi nyumbani
- Mwalimu katwambili kuwa hatasomesha unju - mwalimi ametuambia kuwa hatosemesha asubuhi
- Veye kakumbuku kuwa hekwandika barua - Yeye amekumbuka kuwa hakuandika barua
- Mie nivu hadhani kuwa unapika chakula - Mimi nilidhani kuwa unapika chakula
- Nyuye hamuamini kuwa sakuja jioni - Nyinyi hamuamini kuwa nitakuja jioni

Kama inavyoonesha katika Kitumbatu kishazi tegemezi kinachotumika ni (kuwa/kwamba). Katika tungo hizo kishazi tegemezi kikiondolewa kutakuwa hakuna ukamilifu wa kimuundo, hali hii inajitokeza iwapo vitatumika vitenzi (ambia); (sema); (kumbuka). Tungo hizo hapo juu pia zinaonesha kuwa vishazi vitegemezi hivyo vina uhusiano maalum wa utawalia na utangulizani. Kirai kitenzi kinatawala kishazi tegemezi na sentensi. Aidha, Kitenzi hicho pia kinatangulia vipashio vingine ambavyo vinaandamana na Kitenzi hicho. Vipashio hivyo ni kishazi tegemezi, kitenzi na kielezi kama inavyonekana kwenye mfano ufuatao:



Hata hivyo wakati mwengine kishazi tegemezi si cha lazima, yaani kinaweza kuondolewa na bado muundo wa kirai kitenzi ukawa umekamilika kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

(a) Mwalimu **katwambili** hatasomesha unju - Mwalimu **katuambia** hatasomesha asubuhi

(b) Veo **waseme** hawatakulya - Wao **wamesema** hawatokula

(c) Veye **kakumbuku** hekwandika barua - Yeye **amekumbuka** hakuandika barua

(d) Mie **nivu** hadhani **kwanjika** chakula - Mimi **nilidhaniunapika** chakula

(e) Ali **kawachekehewevyeza** soma - Ali **aliwacheka** hawakuweza kusoma

Katika Kitumbatu tungo hizo ni zile ambazo zimekozeshwa.

(vi) Kirai Kitenzi Chenye Kitenzi, Kirai Kishazi, Kijalizo, Nomino na Sentensi

Kirai hiki ni kirai ambacho kimebeba kitenzi ambacho ni kitenzi kikuu, Kirai nomino ambacho kinaweza kuwa nomino na Kivumishi, kijalizo pamoja na sentensi. Katika lahaja ya kitumbatu mfuatano wa vipashio vya aina hiyo unaonekana katika mfano ufuatao: Shengazi kamwambili kwamba dada ende sokoni



Mchoro huo unaonesha muundo wa Kirai kitenzi kilichotajwa hapo juu. Katika mchoro huo KN inatawala vipashio vilivyo chini yake ambavyo ni pamoja na KT, S, KN na KE. Katika mfuatano huo T inatangulia N, kij na E. Hivyo basi, vipashio vinavyotawaliwa na KN vina uhusiano wa utangulizi na KT inatawala vipashi vilivyo chini yake. Hivyo basi, vipashio vinavyotawaliwa na KT vina uhusiano na utangulizani.

Kirai Kitenzi Chenye Kitenzi + Kirai Kihusishi (KT----------T+KH)

Kirai kihusishi ni kirai ambacho hudokeza uhusiano wa vitu viwili au zaidi. Katika Miundo ya kirai kitenzi pia kuna miundo ya kirai na kihusishi. Katika kirai hicho kuna kihusishi na kirai nomino; hivyo KT inatawala T na KH ambapo H ni kirai kihusishi, wakati T inatangulia vipashio vinavyoandamana na kirai kitenzi kihusishi. Muundo huu unajidhihirisha katika mfano ifuatayo:

Kajifichi chini ya mjiti – Amejificha chini ya mti.



Mifano mingine ya kirai kitenzi na kihusishi

a. Wangili **kati ya** shimo - Wameingia **ndani ya** shimo

b. Vua inyi **wakati wa** ibada - Mvua imenyesha **wakati wa** ibada

c. Kanchora **juu ya** ubao - Anachora **juu y**a ubao

Sehemu zilizokozeshwa ndio vihusishi vya tungo hizo.

(viii) Kirai Kitenzi Chenye Muundo wa Kitenzi na Kielezi (K ---------- T +KE)

Katika Kiswahili Sanifu kirai kitenzi cha namna hii kinaonekana katika mifano ifuatayo:

- A naimba vizuri
- Analia sana
- Anakula haraka

Katika lahaja ya Kitumbatu kirai kitenzi chenye muundo wa kitenzi na kielezi kinaonekana katika mifano ifuatayo:

- Mtoto kankulya haraka - Mtotoa anakula haraka



Mifano mingine ni kama ifuatayo:

a. Kancheka sana - Anacheka sana

b. Twancheza uzuri - Tunacheza vizuri

b. Kansoma haraka - Anasoma haraka

4.2.2 Vipashio Vinavyoandama na Kirai Kitenzi cha Lahaja ya Kitumbatu

Vipashio vinavyounda kirai kitenzi husika huwa na mahusiano maalum ambayo yanaleta uhusiano wa utawala wa moja kwa moja ambapo kiamba jengo katika kifundo cha juu hutawala viambajengo vidogo vya chini yake (Masoud,2011). Aidha, uhusiano wa utangulizani ni wa kisafu wa viamba jengo vidogo vinavyotawaliwa na kifundo kimoja kilicho juu. Kiamba jengo kidogo kimoja hutangulia kiambajengo kidogo kingine katika mfuatano wa kisarufi. Kwa ajili ya kuleta ukamilifu wa tungo, mfano wa vipashio vya aina hiyo ni kama ifuatavyo:

Namba	**Kitenzi**	**Vipashio vinavyoandamana na kitenzi**	
i.	T		
ii.	T	KN	
iii.	T	KN	KN
iv.	T	Ts	T
v.	T	K/kij	S
vi.	T	KN	K/kij + S
vii.	T	KH	
viii.	T	KE	

4.2.3 Sentensi za Lahaja ya Kitumbatu na Muundo Wake

Uchambuzi wa sentensi katika lugha ya Kiswahili umefanywa na wataalamu mbalimbali kama vile Matinde (2012) ambaye alianza kutoa maana ya sentensi kwa kusema:

*"*Sentensi ni nenoaufungu la manenolenye uarifishaji mkamilifu. Sentensi huwana muundouliokamilika na hujitegemeakimaana*"*.

Katika uchambuzi huo wameonyesha miundo mbalimbali ya sentensi inayojitokeza katika lugha ya Kiswahili. Miundo hiyo ni kama hii ifuatayo

- Sentensi sahili
- Sentensi changamano.
- Sentensi ambatano.

Muundo wa sentensi kama huu pia umejitokeza kwenye lahaja ya Kiswahili ya Kitumbatu ambapo ndio malengo yaliyokusudiwa katika utafiti huu kuchunguuza miundo ya sentensi za lahaja ya Kitumbatu. Katika utafiti huu miundo hiyo imechunguuzwa ambapo imedhihirika kuwa sentensi zimegawika katika aina tatu.Aina hizo za sentensi ni hizi zifuatazo:

- Sentensi sahili,
- Ssentensi changamano na
- Sentensi ambatano.

4.2.3.1 Sentensi Sahili

Wataalamu wengi wametoa maana ya sentensi sahili, miongoni mwa wataalamu hao ni (Matinde 2012) ambae ameeleza kuwa sentensi sahili ni sentensi ambayo imeundwa na kishazi huru kimoja ambacho maana yake ni kamilifu.Mara nyingi

sentensi sahili huwa na muundo wa kiima na kiarifu.Pia sentensi sahili huwa na wazo moja.

Muundo wa sentensi sahili za Kiswahili sanifu ni ule ule uliojitokeza katika lahaja ya Kiswahili ya Kitumbatu baada ya mtafiti kupata matokeo ya data alizozichambua kutoka kwa watafitiwa aliowachagua. Muundo huo ni ule wenye kikundi kimoja cha taarifa chenye kudhihirika kwenye kitenzi ndani ya tungo kama inavyoonekana katika mifano ifuatayo:

Sentensi zalahaja ya Kitumbatu	**Sentensi za Kiswahili sanifu**
Mama kanshona nguo	Mama anashona nguo
Veye ni mwazimi buku lyangu	Yeye nimemwazima buku langu
Dada kananjika mhogo	Dada anapika muhogo
Asha kankwimba nyimbo	Asha anaimba nyimbo

Muundo mwengine unaojitokeza katika lahaja ya Kiswahili ya Kitumbatu ni kuwa kuna baadhi ya sentensi sahili ambazo sehemu inayokaliwa na nomino huwa kapa, na nomino hiyo hudhihirishwa na viambishi vya nafsi au nomino ambayo haitajwi kwasababu inaeleweka.

Mifano ya sentensi hizo ni kama hii ifuatayo:

(i)	Kaja	-	amekuja
(ii)	Wampigi Mwalimu	-	wamempiga mwalimu
(iii)	Tucherewa	-	tumechelewa
(iv)	Katatuka zawadi zetu	-	atatupazawadi zetu

Sentensi sahili zinazoonekana hapo juu ni sentensi ambazo nomino zake ni kapa ambazo hazikudhihirishwa. Utafiti huu pia uliona kuwa sentensi sahili za kitumbatu zina miundo ya sentensi ambayo huweza kuwa na yambwa mbili kama inavyoonekana kwenye mifano ifuatayo:

(i) Mama kamnywese mtoto uji - Mama amemnywesha uji mtoto

(ii) Mwalimu kamki kitabu mwanafuzi - Mwalimu amempa kitabu mwanafunzi

(iii) Dakitari kamtoogo mgonjwa shindano - Daktari amemchoma mgonjwa sindano

Wakati mwengine Lahaja ya Kitumbatu hutumia vitenzi kadhaa ambavyo vyengine huwa sio viini vya taarifa.Mfano ni kama ifuatavyo:

(i) Veye kavu akoga - Yeye alikuwa anakoga

(ii) Nyafu kantaka kulya - Nyafu anataka kula

(iii) Nyuye mnapenda kwimba - Nyinyi mnapenda kuimba

4.2.3.2 Sentensi Ambatano katika Kitumbatu

Sentensi ambatano ni sentensi ambayo huwa na vishazi huru viwili au zaidi ndani yake .Vishazi huru ambavyo navyo huwa ni sentensi sahili huambatana kwa kutumia viunganishi (Habwe na Karanja, 2004). Omandi (1992) ambaye amenukuliwa na Habwe na Karanja anaeleza kuwa ili sentenesi iwe ambatani vishazi huru lazima viwe vinachukuana kimaana. Mfano wa sentensi hiyo ni huu ufuatao:

Jane anacheza mpira hali Mary analia.

Kwa mujibu wa data zilizochambuliwa katika utafiti huu, utafiti umegundua kuwa katika sentensi ambatano za lahaja ya Kitumbatu kuna muundo wa sentensi ambao sentensi huunganishwa kwa viunganishi kama vile ‘na’, ‘ama’ na ‘wala’. Viunganishi

hivi huunganisha sentensi sahili mbili, kiunganishi ‘ama’ huunganisha sentensi zinazo kinzana na kiunganishi ‘wala’ huunganisha sentensi ambazo kwa kawaida huwa zina ukanushi. Mifano ya Sentensi kama hizo ni:

(i) Veo hawasikizi wala hawandiki	-	Wao hawasikilizi wala hawaandiki.
(ii) Mama kanlima na baba kanapanda	-	Mama analima na baba anapanda
(iii)Nyambia kutakwenda ama hutakwenda	-	Niambie kama utakwenda ama huendi

4.2.3.3 Sentensi Changamani katika Lahaja ya Kitumbatu

Sentensi changamani ni aina ya sentensi ambayo huundwa na vishazi viwili, kimoja kikiwa huru na kingine tegemezi (Matinde 2012). Miundo ya aina hii pia hujitokeza katika sentensi za lahaja ya Kiswahili ya Kitumbatu ambapo sifa kuu ya sentensi hizi nikuwa na matumizi ya viambishi rejeshi kama{po}, {-o-}na{-ye-}. {-vyo}, na {-yo}. Viambishi hivi ni vile vile vinavyopatikana katika Kiswahili sanifu. Sentensi changamano za lahaja ya Kitumbatu zimegawika katika aina mbili, aina hizo ni sentensi changamani zenye urejeshi na sentensi changamani masharti.

4.2.4 Sentensi Changamani zenye Urejeshi

Hizi ni sentensi ambazo huwa na urejeshi ndani yake. Mifano ya sentensi hizo ni hii inayofuata:

Kitumbatu		**Kiswahili Sanifu**
(i) Mwanamke a**ye**ja jana katoroko	-	Mwanamke aliyekuja jana ametoroka
(ii) Baba a**po**kuja hetwemona	-	Baba alipokuja hatukumuona
(iii) Watoto wa**o**ja leo ni wadugu	-	Watoto waliokuja leo ni wadogo

(iv)	Viazi wa**vyo**panda viozo	-	Viazi walivyopanda vimeoza
(v)	Mahindi tu**yo**vuna yaligwa ni ndudu	-	Mahindi tuliyovuna yameliwa na wadudu

Maneno yaliyokozeshwa hapo juu kuanzia sentensi ya kwanza mpaka ya tano ndio viambishi rejeshi kwenye sentensi changamano hizo za lahaja ya Kiswahili ya Kitumbatu.

4.2.6 Sentensi Changamani Masharti

Hizi ni sentensi changamani ambazo hutumia maneno kama 'hata', 'nge', 'kama' n.k. Mifano ya sentensi hizo ni kama ifuatavyo:

	Kitumbatu		**Kiswahili Sanifu**
(i)	Kama kucharudi tutakungoja	-	Kama utarudi tutakusubiri
(ii)	Hata ukampiga hatakulya	-	Hata ukimpiga hatokula
(iii)	Ungemwita angekuja	-	Ungelimuita angekuja

4.2.7 Vitenzi Elekezi katika lahaja ya Kitumbatu

Vitenzi elekezi ni vitenzi ambavyo huhitaji yambwa ili kuleta maana kamilifu (Matinde 2012). Ameendelea kusema kuwa bila yambwa vitenzi hivi havina uarifishaji mkamilifu. Hata hivyo kimantiki vitenzi hivi huwa na yambwa mahsusi ambazo huendana nazo.Habwe na Karanja (2004) wanaeleza kuwa vitenzi elekezi ni vitenzi ambavyo huashiria kitendo na hali ambayo huruka mipaka na kuathiri maneno mengine ya sentensi.Maneno haya yanayoathiriwa huwa ni yambwa tendwa au tendewa.Mifano ya vitenzi hivyo inaonekana katika sentensi zifuatazo:

Kitumbatu		**Kiswahili Sanifu**
(i) Mwalimu kandiki kitabu	-	Mwalimu ameandika kitabu
(ii) Paka kamgwili panya	-	Paka amemkamata panya
(iii) Murshid kanywi chai	-	Murshid amekunywa chai

Vitenzi {kandiki}, {kamgwili}, na {kanywi} vilivyotumika katika sentensi hizi ni elekezi. Hii ni kwasababu vitendo vya vitenzi hivi huathiri yambwa katika sentensi zilizo hapo juu. Vitenzi hivi vinaonekana kuandamana na nomino moja ambapo nomino hizo zinaweza kuwa ni jina la kitu, mtu, mnyama au sehemu. Kitenzi 'kandiki' kimeandamana na jina la kitu, na kitenzi 'kamgwili' kimeandamana na jina mnyama. Hivyo basi vitenzi hivyo ni elekezi kwani bila ya kuwepo kwa nomino hizi havitakamilika kimuundo na kimatumizi. Mchoro ufuatao unaonesha mfano wa maelezo ya hapo juu:



Pia katika vitenzi elekezi vipo vitenzi ambavyo hufuatiwa na nomino mbili ambavyo huitwa elekezi mara dufu. Mifano ya vitenzi hivyo ni:

Kan watilia watoto chakula



Mifano mengine ni:

Kitumbatu		**Kiswahili Sanifu**
(i) Bibi **kan-wahadithia** watoto hadithi	-	Bibi anawatolea watoto hadithi
(ii) Mwalimu **kam-nunulili** mwanafunzi zawadi	-	Mwalimu amemnunulia mwanafunzi zawadi
(iii) Asha **kamgaili** Aziza bulpeni	-	Asha amemgaiya Aziza Kalamu
(iv) Tatu **kanampikia** mama ugali	-	Tatu anampikia mama ugali

Yeye amemgaia motto pesa

Vitenzi viliokozeshwa ndivyo maradufu kwani mbele yake zinaonekana nomino mbili

Vitenzi Visoelekezi (<sie>)

Vitenzi visoelekezi ni vitenzi ambavyo kimantiki havihitaji yambwa kudokeza uarifishaji mkamilifu. Pia vitenzi hivi vinaweza kufuatiwa na vipashio vingine kama vile kielezi. Mfano wa tungo za vitenzi hivi inafuata chini:

Mtoto kanlia usiku



Mfano wa hapo juu unaonekana kuwa kitenzi hicho sio elekezi lakini kimeandamana na kielezi. Mifano ifuatayo hapo chini inaonesha vitenzi sio elekezi ambavyo havijaandamana na nomino wala kielezi.

Mfano wa vintezi hivyo ni:

a. Kagu - ameanguka

b. Kafurahi - amefurahi

c. Karudi - amerudi

d. Kafu - amefariki

e. Kantabasamu - anatabasamu

Uelekezi unahusishwa pia katika utafiti huu kutokana na kuwepo kwake katika kirai kitenzi kama ambavyo itadhihirika kuwa na nomino moja au mbili kwenye sentensi. Hivyo, kitenzi elekezi ni kitenzi ambacho kutokana na umbile lake kinahitaji kukamilishwa na nomino, kitenzi kinachofuatwa na nomino mbili kinajuilikana ni elekezi maradufu.

4.3 Hitimisho

Katik a uchambuzi uliofanyika hapo juu tumeweza kubainisha miundo tafauti ya virai vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu pamoja na vitenzi elekezi na visivyoelekezi vya lahaja hiyo.

SURA YA TANO

MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, HITIMISHO LA JUMLA NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika sura hii tulieleza kwa ufupi yote yaliyojitokeza katika tasnifu hii, kwa kueleza matokeo yaliyogunduliwa katika utafiti huu.Mwisho surah ii imetoa mapendekezo yaliyopendekezwa na mtafiti.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Sura ya kwanza ilieleza kuwa wataalam mbalimbali walifanya utafiti katika lahaja ya Kitumbatu kwa vipengele mbalimbali, lakini hakuna utafiti uliofanywa kuhusu kirai kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu,hivyo mtafiti ameamua kulichunguza tatizo kiundani. Katika surah ii tulieleza malengo ya utafiti pamoja na maswali ya utafiti ambayo yalituongoza katika ukusanyaji data zitakazofanikisha malengo yetu.

Malengo ya utafiti huu yalikuwa matatu nayo ni kuchunguza miundo na vipashio vinavyoandamana na kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu,kuchunguza miundo ya sentensi za lahaja ya Kitumbatu na mwisho nikubainisha uelekezi unavyojitokeza katika vitenzi vya lahaja ya Kitumbatu.

Sura ya pili ilionesha kazi tangulizi ambazo zinahusu lahaja ya Kitumbatu na zinazohusu Kiswahili sanifu.Mwisho w asura hii tulitaja kiunzi cha nadharia ambacho kimetumika katika utafiti huu ambacho ni nadharia ya sarufi jumuishi ya muundo virai ambayo mwanzilishi wake Gerald Gazdar ambae alipata mchango kutoka kwa Ivan Sag na Ewan Klein.

Sura ya tatu ilihusu eneo la utafit, sampuli ya utafiti,mkabala wa utafiti,mbinu za utafiti na uteuzi wa sampuli ambapo katika utafiti huu umefanywa kwa watafitiwa wenye umri wa miaka 70. Mwisho utafiti huu umetumia mbinu ya dodoso ambayo ilitolewa kwa watafitiwa ilikutoa data zilizo sahihi.

Sura ya nne ilikuwa na uchambuzi wa data ambao ulionesha kuwa katika lahaja ya Kitumbatu kuna miundo ya sentensi ya aina tatu ambayo ni sentensi sahili, ambatano na changamano.Vilevile kuna miundo mbalimbali ya kirai kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu,pia kuna vitenzi ambavyo ni lazima vifuatiwe na nomino moja au mbili na vitenzi vyengine haviwezi kufuatiwa nanomino katika ukamilifu wake.

5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza muundo wa kirai kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu,ambao umeegemea zaidi katika kuangalia vipshio vinavyoandamana na kirai kirai cha lahaja hiyo. Mtafiti amependekeza kufanyika utafiti ambao utaangalia tofauti ya matumizi ya lahaja ya Kitumbatu kati ya wanawake na wanaume, na vipengele mbalimbali vya kiisimu vya lahaja ya Kitumbatu.

5.4 Hitimisho

Utafiti huu ulionesha miundo mbalimbali ya kirai kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu, vipashio vinavyoandamana nacho na miundo ya sentensi pamoja na kuangalia vitenzi vya lahaja hiyo vinayokuwa.Kuonesha nadharia iliyotumika katika kuchunguza miundo ya kirai kitenzi cha lahaja ya Kitumbatu. Mwisho kabisa ni kutoa mapendekezo ya utafiti. Matumaini yetu kwamba utafiti huu utaongeza ari kwa watafiti wengine kufanya tafiti zaidi kuhusiana na lahaja za Kitumbatu kwa lengo la kupunguza pengo lililopo kuhusiana na lahaja hiyo

MAREJELEO

Ahmad, K. (2003). *Lahaja za Kiswahili.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

BAKIZA, (2012). *Kamusi la Lahaja la Kitumbatu.* Dar es Salaam: Jamana Printers Ltd.

Goode, W. J., & Hatt, P. K. (1952). *Methods in Social Research.* Tokyo: Mc Groww –Hill Book Company Inc.

Habwe, J., na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Masebo, J. A., na Nyangwine, N. (2007). *Nadharia ya Lugha. Kiswahili 1*: Dar es Salaam : Nyambari Nyagwine Publisher

Kihore, Y. M. (2003). *Sarufii Maumbo ya Kiswahili Sanifu*: (SAMAKISA), Sekondari na Vyuo. Dar es Salaam; TUKI.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology. Methods and Techniques Reviesed 2nd Edition*. New –Delhi: New Age International (P) Limited Publishers.

Kothari, C. R. (1990). *Research Methods; Methods and Techniques.* New Delhi: Wiley Eastern.

Maganga, C. (1991). Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi. A study of Mophonology of Standard Kiswahili, Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu.Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa), Dar es Salaam, Tanzania

Makame, K. O. (2012). "Muundo wa virai nomino katika Kitumbatu".Tasnifu ya Shahada ya Shahada ya Uzamivu; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa), Dar es Salaam, Tanzania.

Masoud, N. (2011). “Muundo wa Kiraii Kitenzi katika lugha ya kisambao”. Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. (Haijachapishwa), Dar es Salaam, Tanzania

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia.* Kwa Sekondari na Vyuo vya Kati naVyuo Vikuu. Serengeti Educational Publishers (T) Mwanza. Tanzania.

Matinde, R., Buliba, A., na Gwachi, M. (2012*). Misingi ya Nadharia naMbinu z Utafiti.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Mgulu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahii.* Nairobi: Longhon Publishers.

Miraji, J. (2015). “*Kupunguakwa matumizi ya lahaja ya Kitumbatu”*.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo cha Kumbukumbu ya Abdul Rahman Alsumait Chukwani Zanzibar. (Haijachapishwa), Zanzibar, Tanzania.

Omond, L. N. (1992). *Linguist (Part III).* Nairobi:University of Nairobi Press.

Stigand, C. H (1915). *A Grammmar of Dialect Changes in Kiswahili Language.* Cambridge: Cambridge University Press.

Stude, T. (1995). “Language Change and Language Maintenance of the Island of Tumbatu. (83 -115) (katika Mlacha, SAK na A. Hurslinen), Lugha Utamaduni na Fasihi ya Kiswahili. Zanzibar, Tanzania.

KIAMBATISHO

Kiambatisho I:Hojaji za Muundo wa Virai Vitenzi katika Lahaja ya Kitumbatu

Tafadhhali unaombwa kujibu maswali yafuatayo kadri ya uelewa wako:

SEHEMU YA KWANZA: MAELEZO BINAFSI

1. Jina:…….....
2. Jinsia:…….....
   .
3. Kiwango chako cha Elimu:.....
4. Umri:.....……
5. Kijiji Unachoishi:.....
6. Miaka ningapi umeishi katika kijiji hiki:.....

SEHEMU YA PILI

Katika mwali yafuatayo badilisha sentensi zifuatazo kwenda katika lahaja ya Kitumbatu

1. Amepoteza simu:…….…….....
2. Mwalimu ametuambia kuwa hatosemesha asubuhi:…….…….....……
3. Daktari amemchoma mgonjwa sindano:.....……...……
4. Anasoma haraka:……..…….....
5. Amekuja:.....…… …….
6. Mama anashona nguo:.....……
7. Wao hawasikilizi wala hawaandiki:.....……

8. Amejificha chini ya mti:.....……

9. Ataweza kusoma:.....……..

10. Mama analima na baba anapanda:.....……

11. Mwanamke aliyekuja jana ametoroka:.....…….……

12. Mahindi tuliyovuna yameliwa na wadudu:.....……

13. Ameanguka:.....…… ……..

14. Paka amemkamata panya:.....……

15. Baba amerudi:.....……

16. Yeye ni memuazima buku lang:.....……

17. Nyafu anataka kula:.....…… ……

18. Mama anawatilia watoto chakula:…….....

19. Mtoto analia usiku:…….. …….....

20. Mwalimu ameandika kitabu:.....……..……...…….

21. Murshid amekunywa chai:……..…….....

22. Wao wamesema hawatokula:……...…….....

23. Mama anamnywesha uji mtoto:…….....

24. Tutamuangalia:.....… …..…….

25. Shangazi amemwambia dada kwamba aende sokoni:……..……

26. Mwalimu amemnunulia mwanafunzi zawadi:……,,,,,,……

27. Wanafunzi wanasoma na kuandika:……..…….

28. Baba amesema kwamba anaenda mjini:...……

29. Kama utarudi tukusubiri?:.....…….....……..…….

30. Mtoto amelalamika kwamba amelazimishwa kwenda Skuli:.....……

31. Amemfanyia mwalimu kelele:.....…….… …… …….

32. Watoto waliokuja leo wadogo:.....

33. Amemkamata mwizi:.....

34. Amemnunulia mwanafunzi kalamu:.....

35. Nilikuwa nikilima:.....

SEHEMU YA TATU

Sentensi zifuatazo ni za lahaja ya Kitumbat, zibadilishe kuwa Kiswahili Sanifu

1. Wampigi mwalimu:…….…….……..

2. Kachatuka zawadi zetu:……...……

3. Mwalimu kamki mwanafuzi kitabu:……..…….

4. Vua inyi wakati wa ibada:…….……..……...…….

5. Kancheka sana:……..…….

6. Kanchora juu ya ubao:……...……..

7. Dakitari kamwambili baba kwamba mgonjwa arudi:…….…..……...

8. Wankulya ubwabwa:……..…….

9. WAnchaka kwandika:……..…...…….

10. Wangili kati ya bonde:……...…….…….

11. Veye kakumbuku kuwa hekwandika barua:…...……

12. Kankokeza:…….....

13. Kafu:……

14. Wanauka:……

15. Kachukuu kuku:……..
16. Wancheza mpira:……..……..
17. Kanjiki mhogo:……..……..
18. Wamki mwana zawadi:……..……..
19. Wampenda kwandika:……..……..
20. Kavuakoga:……..…….
21. Veye kakumbuku kuwa hekwandika barua:…….
22. Mtoto kankulya haraka:……..
23. Twancheza uzuri:….……..
24. Asha kankwimba nyimbo:……..
25. Tucherewa:……..
26. Veye kavu akoga:……..……..
27. Nyuye mwanpenda kwimba:……..
28. Nyambia kutakwenda ana hutakwenda:……..
29. Baba apokuja hetwemona:……..
30. Viazi wavyopanda viozo:……..
31. Hata ukampiga hatakulya:……..
32. Ungemwita angekuja:……..……..
33. Bibi kan wahadithia watoto hadithi:……..
34. Asha kamgaili Aziza kalamu:……..
35. Kafurahi:……..

Nashukuru sana kwa mashirikiano yako